



CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255622470751, S.L.P. 708, Arusha, T.Z. kingoriteachers@yahoo.com, www.kingoriteachers.com

Tar./....../2026

KUMB.NA. KTC/CU.118/E0623/'26/ ...

Ndugu

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE ZA MSINGI

Uongozi wa Chuo cha Ualimu KING'ORI unakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa shule za msingi (DIPLOMA IN PRIMARY SCHOOL EDUCATION) katika Chuo cha Ualimu King'ori yatakayochukua miaka miwili. Hongera Sana.

Chuo kitafunguliwa tarehe **28 June 2025** na unatakiwa uwe umeripoti chuoni kabla ya mwezi wa **saba** kuisha kwa ajili ya kuanza masomo mara baada ya zoezi la usajili kukamilika. Soma kwa makini MAELEZO, MAAGIZO na MASHARTI ya kujiunga na chuo hiki kabla ya kukamilisha usajili wako.

Uongozi wa chuo unakupongeza sana na kukutakia kila la kheri na maandalizi mema.

Tunakukaribisha kwa furaha kujiunga nasi.

.....
PAUL ISACK NGOWI
MKUU WA CHUO





CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255622470751, S.L.P. 708, Arusha, TZ. kingoriteachers@yahoo.com, www.kingoriteachers.com

MAELEZO, MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA CHUO

CHA UALIMU KING'ORI

1. Maelezo

Chuo cha Ualimu King'ori ni chuo cha kutwa na Bweni. Chuo kinatoa mafunzo ya Ualimu ngazi ya **Stashahada ya Ualimu wa Shule za Msingi** (Diploma in Primary Education). Tunafuata Mitaala na Mihtasari iliyokubaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Chuo kimesajiliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa usajili na. CU118 na Baraza la Mitihani Tanzania kwa usajili na. E0623.

Chuo kinawaandaa wanachuo ili wawe walimu bora katika Shule za Msingi na Sekondari na katika jamii kwa ujumla. Chuo kinamilikiwa na mtu binafsi na kinapokea wanachuo kutoka maeneo yote Tanzania.

2. Mahali Chuo Kilipo

Chuo cha Ualimu King'ori kipo **Arusha Mjini**, Kata ya Sekei, mtaa wa **Banana**, maeneo ya **Phillips**. Kipo takribani mita 100 kutoka barabara ya Arusha-Moshi kando ya barabara iendayo Mahakama ya Wilaya ya Arumeru.

3. Kufungua Chuo

- (a) Chuo kitafunguliwa tarehe **28/June/2025** kwa ajili ya wiki ya maelekezo (Orientation week) pamoja na kukamilisha Usajili kwa wale ambao watakuwa bado hawajakamilisha. Mafunzo ya Ualimu yataanza rasmi tarehe **06/07/2025** baada ya wiki hiyo ya maelezo na kukamilisha usajili. Unatakiwa uwe umekamilisha usajili wako kabla au ifikapo tarehe **06/07/2025**.

TANBIHI : Kama kutakuwa na mabadiliko ya tarehe ya kufungua chuo, utajulishwa kwa njia ya simu au Kupitia tovuti ya chuo.

4. Sifa za kujiunga na Utambulisho wa Muombaji

Ili kuthibitisha kuwa wewe ndiye HALISI ambaye unajiunga na mafunzo ya Ualimu katika chuo hiki, itakubidi uje na viambatanisho vifuatavyo;

- (a) Cheti halisi cha kumaliza mafunzo/elimu ya kidato cha IV na VI (Original School Leaving Certificate) kikionyesha shule uliyosoma na cheti halisi cha matokeo ya mitihani ya **kidato VI** cha Baraza la Mitihani la Tanzania (BMT) **au** Cheti cha Ualimu cha **Daraja la IIIA**.
- (b) Nakala **mbili** (2) za picha yako ndogo (passport size) za rangi, ulizopiga hivi karibuni.

5. Kusajiliwa

Usajili utafanyika chuoni baada ya kuwasilisha Nyaraka za utambulisho tajwa katika kipengele **namba 4** katika ukurasa wa pili hapo nyuma.

6. Masharti Mengine Muhimu

a). Taaluma

Chuo kinaweka msisitizo wa kipekee katika maendeleo ya wanachuo wake kitaaluma. Kiwango cha kufaulu kwa wanachuo katika kila somo ni alama 50. Kwa wanachuo wa michepuo yote, endapo utashindwa kufikia kiwango hicho mwishoni mwa muhula wako wa kwanza utalazimika kufanya mtihamu wa marudio (Supplementary Examination). Ukishindwa tena mtihamu huo, utashauriwa utafute kozi nyingine tofauti na Ualimu.

Vilevile tunao walimu wakutosha na mahiri katika ufundishaji. Mtihamu hii ni njia mojawapo ya kuinua UBORA NA HADHI YA UALIMU NCHINI. Hivyo mwanachuo anashauriwa aje chuoni akiwa anajielewa fika kuhusu uwezo wake wa kumudu masomo atakayo chukua. Atatakiwa aweke mkazo kwenye masomo tangu siku anapoingia chuoni.

Pia, wanachuo watakapokuwa wakiendelea na masomo yao watapewa maelezo ya namna ambavyo zoezi la kufundisha kwa vitendo litakavyofanyika.

b). Kanuni za Chuo

Pamoja na maelezo haya na masharti ya kujiunga na chuo utapewa taratibu na kanuni za kukusaidia kuishi vizuri hapa chuoni. Hakikisha umezisoma, umezielewa, na unakubaliana nazo kabla ya kusajiliwa.

c). Ada

Ulipaji wa Ada ya Chuo umegawanywa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini, kumrahisishia Mwanachuo / Mzazi / Mlezi ulipaji. Mwanachuo / Mzazi / Mlezi anaweza kulipa Ada yote ya mwaka mzima bila kujali mgawanyo huu.

 ***Baada ya kusoma, kuelewa na kukubaliana na masharti ya kujiunga na Chuo hiki, jaza na usaini kurasa mbili za mwisho za fomu hii na kisha uziwasilishe ofisini kwa msajili wakati utakaporipoti.***





CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255622470751, S.L.P. 708, Arusha, TZ. kingoriteachers@yahoo.com, www.kingoriteachers.com

KANUNI / MASHARTI YA CHUO

- 1) Kila mwanachuo lazima ahudhurie na kuwahi vipindi vyote vilivyopangwa katika ratiba.
- 2) Mwanachuo ataachishwa mafunzo asipohudhuria 1/3 [theluthi] ya idadi ya vipindi katika muhula mmoja.
- 3) Hairuhusiwi kwa mwanachuo kuja chuoni akiwa ametumia kileo au kutumia aina yoyote ya kileo akiwa chuoni. Adhabu yake ni kufukuzwa chuo
- 4) Mwanachuo lazima kuwa mwaminifu kwa kutunza na kulinda mali ya umma na ya mwenzake. Wizi utapelekea kuachishwa mafunzo kwa mwanachuo. Aidha uharibifu wa mali za chuo adhabu yake ni kulipa .
- 5) Hairuhusiwi kuingia ofisini, darasani au chuoni ukiwa umevaa; bukta za michezo, kandambili, kanga, dela, nguo zinazobana, nguo za usiku na kofia. Nguo zisizo za heshima ni marufuku katika mazingira ya chuo.
- 6) Mikutano, vikao vya wanachuo vitafanyika kwa kibali cha Mwadili wa chuo na Mkuu wa chuo, kufanya mikutano na vikao bila kibali adhabu yake ni kuachishwa mafunzo au kufukuzwa chuo.
- 7) Kugoma au kuchochea watu waingie katika mgomo ni kosa kubwa, adhabu yake ni kuachishwa mafunzo.
- 8) Barua za kiofisi au makala yoyote inayopelekwa kwenye vyombo vya habari, lazima ipitishwe kwa Mkuu wa chuo.
- 9) Ruhusa hutolewa na kati ya hawa wafuatao :

{a} Mkuu wa chuo	{b} Makamu Mkuu wa chuo
{c} Mwadili	{d} Mkufunzi wa zamu
{e} Mwalimu wa darasa.... Kwa kumtaarifu kwanza mwalimu wa zamu .	
- 10) Kuwa nje ya darasa bila ya sababu za msingi ni marufuku. Adhabu yake ni kusimamishwa masomo.
- 11) Unapokuwa darasani na unataka kutoka nje unapaswa kuomba ruhusa kwa Mkufunzi aliyeko darasani kwa wakati huo. Vinginevyo utaadhibiwa.
- 12) Kila mwanachuo lazima awe na nidhamu ya hali ya juu kwa kutii wadogo kwa wakubwa. Bila nidhamu utasimamishwa masomo .
- 13) Kila mwanachuo aheshimu uongozi wa chuo yaani Mkuu wa chuo, Wakufunzi wote, Serikali ya Wanachuo na yeyote aliye mfanyakazi wa chuo na wanachuo wenzake
- 14) Kila mwanachuo ni lazima aheshimu mali zake, za chuo na za wanachuo wengine wote.
- 15) Uhusiano wa aina yeyote ile wa kimapenzi kati ya mwanachuo na mwanachuo, mwanachuo na mkufunzi au mwanachuo na mfanyakazi yeyote wa chuo hauruhusiwi. Adhabu yake ni kufukuzwa chuo.
- 16) Uvutaji wa sigara na matumizi ya madawa ya kulevya ni marufuku. Adhabu yake kufukuzwa chuo.
- 17) Mijadala, kongamano, mikutano ya kisiasa, masuala ya dini na ukabila ndani ya chuo haviruhusiwi vinginevyo muhusika ataondolewa chuoni mara moja.
- 18) Ugomvi, kupigana, kutukana kwa namna yoyote ni marufuku. Adhabu yake kufukuzwa chuo.
- 19) Ni marufuku kwa mwanachuo kutumia simu wakati wa masomo isipokuwa kwa kuruhusiwa na mkufunzi.



CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255622470751, ☒ S.L.P. 708, Arusha, TZ. ✉ kingoriteachers@yahoo.com, 🌐 www.kingoriteachers.com

FOMU YA KUJIUNGA NA CHUO CHA UALIMU KUNG'ORI

A. TAARIFA BINAFSI

- | | |
|---------------------------------|--------------|
| (i) Jina kamili | |
| (ii) Anuani | (iii) Wilaya |
| (iv) Mkoa | (v) Simu |
| (vi) Jina la Mzazi/Mlezi: | (VII) Simu |

B. TAARIFA YA ELIMU

- | | | |
|------------------------------------|-------------|-------|
| (i) Shule ya Msingi | Mwaka | Mpaka |
| (ii) Shule ya Sekondari | Mwaka | Mpaka |
| (iii) Elimu ya Chuo (Kama ulisoma) | | |

C. UTHIBITISHO

Mimi nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi.
Jina Sahihi Tarehe

Kwa Matumizi ya Ofisi tu

Maoni ya Mkuu wa Chuo :
.....
.....

Sahihi : Tarehe : Muhuri :



CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255622470751, S.L.P. 708, Arusha, TZ. kingoriteachers@yahoo.com, www.kingoriteachers.com

MKATABA BAINA YA MWANACHUO NA CHUO

Mimi ----- nimesoma na kuyaelewa pia kuyakubali masharti ya kujiunga na chuo hiki pamoja na kanuni zake zote zinazotawala na zinazohusu Malipo ya Ada, Michango ya Ada ya Mitihani, n.k.

Naahidi kuwa:

- Nitayatimiza masharti yote yaliyoandaliwa pamoja na kanuni nyingine zitakazotawala mafunzo yangu hapa chuoni.
- Nitajifunza kwa uwezo wangu wote na kufanya mitihani yote na kufaulu kwa kiwango kilichowekwa na chuo.
- Iwapo nitashindwa kufikia kiwango cha taaluma kilichowekwa au kufanya kosa lolote kubwa kwa mujibu wa kanuni za chuo, nitakuwa nimejiondoa mwenyewe chuoni na hivyo sitadai kurudishiwa kiasi chochote cha fedha nilichokwisha kulipwa.
- Nitaziheshimu sheria za nchi ya Tanzania kama zinavyonihusu.
- Iwapo nitaenda kinyume na kuvunja sheria yoyote ya nchi hii, nitakuwa tayari kupokea na kuchukuliwa hatua zozote za kisheria dhidi yangu.

Sahihi:

Tarehe:

Jina la Shahidi : Sahihi : Tarehe :

Kwa Matumizi ya Ofisi tu

Jina la Msajili :

Sahihi : Tarehe : Muhuri:

